FUNZO LA 4

1. Je, Mungu yuko na mwili, mifupa au damu?
-La.

2. Kama Mungu hana mwili, mifupa au damu, basi Mungu ni nini?
-Mungu ni roho.

3. Mungu yuko wapi?
-Mungu yuko kila mahali wakati wowote.

4. Twaweza kwenda wapi ili tujifiche kutoka kwa Mungu?
-Hatuwezi jificha kutoka kwa Mungu.

5. Kuna Mungu wangapi?
-Kuna Mungu mmoja pekee.

6. Ni nani ambao wako kwa utatu na ni Mungu mmoja?
-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

-Malaika wote walitoka wapi?
-Mungu aliwaumba wote hapo mwanzo.

-Kabla ya mwanzo, hakuna malaika aliyekuwepo.

-Kwa nini Mungu ni mkuu zaidi ya malaika?

-Kwa sababu Mungu alikuwepo kabla ya malaika.
-Kwa sababu Mungu aliwaumba malaika.



-Kwa sababu Mungu aliwapa malaika uhai.
-Kwa sababu Mungu ni mwenye nguvu.

-Mungu alipowaumba malaika, je, aliwapa mwili na damu?
-La.

-Mungu aliwaumba malaika kama roho.

-Mungu ni roho, malaika pia ni roho, lakini Mungu ni mkuu zaidi ya malaika.

-Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Lakini malaika hawana nguvu zote.

-Mungu anaweza kuwa mahali popote wakati wowote.
-Lakini malaika wanaweza kuwa mahali pamoja wakati mmoja.

-Japo Mungu aliumba malaika kama roho, wakati mwingine wao hubadilisha sura yao wakawa kama binadamu.

-Kwa nini Mungu aliumba malaika?

-Je, Mungu alihitaji msaada wowote?
-La.
-Nguvu za Mungu haziishi, ni za milele.

-Kwa nini Mungu aliumba malaika?

-Mungu aliumba malaika ili wampende.
-Mungu aliumba malaika wamtii.

-Mungu aliumba malaika wamtumikie.

-Kama mtu atajenga nyumba, hio nyumba itakuwa ya nani?
-Ya huyo mtu.

-Kwa nini?
-Kwa sababu huyo mtu ndiye aliyejenga hiyo nyumba.

-Kama mwanamke atafinyanga chungu, hicho chungu kitakuwa cha nani?
-Cha huyo mwanamke.

-Kwa nini?
-Kwa sababu huyo mwanamke ndiye aliyekitengeneza.

-Kama Mungu aliumba malaika, ni nani anayemiliki malaika?
-Mungu.

-Kwa nini?
-Kwa sababu Mungu ndiye aliyewaumba malaika

-Kwa sababu Mungu aliwaumba malaika, malaika ni wake.

-Je, Mungu aliwaumba malaika wazuri au wabaya?
-Mungu aliumba malaika wote wazuri.

-Mungu hawezi umba malaika wabaya.
-Mungu hawezi umba chochote ambacho ni kibaya.

-Kila anachowaza Mungu ni kizuri.



-Kila anachosema Mungu ni kizuri.
-Kila anachofanya Mungu ni kizuri.

-Mungu aliumba malaika wangapi?
-Mungu aliumba malaika wengi, hatuwezi kuwahesabu wote.

-Hapo mwanzo, malaika wote waliishi wapi?
-Mbinguni pamoja na Mungu.

-Mbinguni ni wapi?
-Mbinguni ni mahali maalum pa Mungu, mahali ambapo anaishi.

-Mungu yuko Mbinguni, pia Mungu yuko kila mahali hapa duniani.

-Mbinguni iko upande gani?
-Hatujui, lakini iko mbele ya jua, mwezi na nyota.

-Kati ya malaika aliowaumba mungu mmoja alikuwa na hekima nyingi na wa kupendeza sana.

-Jina la malaika aliyeumbwa na hekima kubwa na urembo mwingi ni?
-Lusifa.

-Je, Mungu alimuumba Lusifa mzuri au mbaya?
-Mzuri.

-Mungu anaweza kuumba malaika wazuri tu.

-Mungu hawezi kuumba malaika wabaya.

-Mungu alimuumba Lusifa na hekima kubwa, lakini hekima ya Mungu haiishi.

-Mungu alimuumba Lusifa na urembo mwingi, lakini urembo wa Mungu hauishi.

-Kwa sababu Mungu alimuumba Lusifa, Lusifa alikuwa wa nani?
-Wa Mungu.

-Kwa sababu Mungu alimuumba Lusifa, Lusifa yuafaa kumtii nani?
-Mungu.

-Hapo mwanzo, nini kilimfanyikia Lusifa?

-Lusifa aliona hekima na urembo wake na akajawa kiburi.

-Lusifa alijawa kiburi na akataka kumuondoa Mungu mamlakani.

-Lusifa alijawa kiburi na akataka kuchukuwa nafasi ya Mungu.
-Lusifa alijawa kiburi akataka kuwa Mungu.

-Lusifa akajawa kiburi, akawa wa kwanza kufanya dhambi.

-Nani aliyekuwa wa kwanza kufanya dhambi?
-Lusifa.



-Dhambi ni nini?
-Dhambi ni kitu ambacho Mungu hataki.
-Dhambi ni yote ambayo Mungu hataki.

-Je Mungu alijua kuwa Lusifa alitaka kumtoa mamlakani?
-Ndiyo.
-Mungu aliyajua mawazo yote maovu ya Lusifa.

-Je, Mungu alimkubalia Lusifa kumtoa mamlakani?

-Ufuatao ni mfano:

-Kijiji kimoja kilitawaliwa na chifu aliyekuwa na nguvu na hekima.

-Siku moja, mwanawe mnyonge na mpumbavu akajaribu kumtoa mamlakani.

-Huyo chifu aliyekuwa na hekima na nguvu, je, angemruhusu mwanawe mnyonge na mpumbavu kumtoa mamlakani?
-La.

-Ni nani aliye na nguvu zaidi ya Mungu?
-Hakuna.

-Ni nani aliye na hekima zaidi ya Mungu?
-Hakuna.

-Je, Mungu alimruhusu Lusifa amtoe mamlakani?
-La.

-Kwa sababu Lusifa ndiye aliyekuwa wa kwanza kufanya dhambi, Mungu alibadilisha jina lake.

-Jina mpya la Lusifa ni nani?
-Shetani.

-Jina  Shetani linamaanisha nini?
-Jina  Shetani linamaanisha "adui."

-Shetani ni adui wa Mungu.
-Shetani ni adui wa kila mtu.

-Mungu alimwadhibu vipi Shetani kwa kutenda dhambi?
-Mungu alikasirishwa na Shetani akamwondoa Mbinguni.

-Mungu hawezi kumruhusu yeyote afanyaye dhambi kuishi na yeye.

-Kulikuweko malaika wengi ambao waliungana na Shetani katika uasi wake dhidi ya Mungu.

-Kwa sababu malaika walio mfuata Shetani walimkosea Mungu, Mungu alibadilisha majina yao.

-Je hao malaika waliomfuata Shetani waliitwaje?
-Mapepo.

-Mapepo ni maadui wa Mungu.
-Mapepo ni maadui wa kila mtu.



-Mungu aliwaadhibu aje Mapepo waliomfuata Shetani?

-Mungu alikasirishwa na wao, akawaondoa Mbinguni.

-Mungu hawezi kumruhusu yeyote afanyaye dhambi kuishi na yeye.

-Tena Mungu aliwaadhibu vipi Shetani na Mapepo wake?

-Mungu aliandaa mahali pabaya pa adhabu ya milele kwa Shetani na Mapepo wake.

-Jina la mahali pa adhabu ya milele ni?
-Ziwa la moto wa milele.

-Siku moja, Mungu atawaweka Shetani na mapepo wake katika Ziwa la moto wa Milele.

-Mungu ni mkamilifu na anachukia dhambi.
-Mungu ni mkamilifu, na huadhibu mabaya.

-Shetani na mapepo wake wanaishi wapi sasa?
-Shetani na malaika wake wanaishi duniani sasa.

-Shetani na mapepo wake wanafanya nini sasa?
-Wanapigana dhidi ya kazi ya Mungu mchana na usiku.

-Shetani na mapepo wake wanamchukia Mungu.
-Shetani na mapepo wake wanawachukia watu wote.